1

HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI

MTIHANI WA KIDATO CHA TANO

Muda: Saa 3

Maelekezo

1. Mtihani huu una maswali **saba (7)**.
2. Jibu maswali **matano (5)** tu. Swali la **kwanza (1)** ni la lazima.
3. Kila swali lina alama 20.
4. Maandishi yote yawe kwa wino **mweusi** au **bluu, isipokuwa** michoro, iwe kwa penseli.

Jibu Maswali **Matano (5)**. Swali la **kwanza (1)** ni la lazima.

1. Serikali ya Tanzania imeandaa kongamano la vijana kuhusu uzalendo na utambulisho wa taifa. Wewe umechaguliwa kuwa mtoa mada mkuu. Kwa kutumia mifano hai, eleza vitu sita vinavyolitambulisha Taifa la Tanzania, vinavyojenga na kuimarisha utambulisho wa kitaifa na mshikamano wa wananchi.

2. Wizara ya Maliasili na Utalii imeanzisha kampeni ya "Tambua Urithi Wako" ili kuwahamasisha vijana kuthamini maeneo ya kihistoria. Kama afisa wa wizara hiyo, chambua kwa kina umuhimu wa maeneo ya kihistoria na yenye urithi nchini Tanzania katika kukuza maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa kutumia hoja sita.

3. Serikali inapanga kuendeleza uchumi wa buluu na utalii wa urithi katika maeneo ya pwani kama Kilwa, Bagamoyo na Zanzibar. Fafanua kwa kutumia hoja sita jinsi vivutio vya kihistoria na urithi vinavyoweza kuzalisha fursa za uwekezaji na kuchochea maendeleo ya taifa.

4. Katika semina ya kitaifa ya historia ya Afrika, umeombwa kuwasilisha mada kuhusu maendeleo ya jamii za kale za Tanzania kabla ya ukoloni. Eleza kwa kina vichocheo vya maendeleo katika jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni na namna vilivyochangia ustawi wa jamii hizo.

5.Tafiti zinaonesha kuwa mwingiliano kati ya jamii za Kitanzania na jamii nyingine uliathiri sana maendeleo ya Afrika Mashariki. Kwa kutumia hoja sita, chambua kwa kina matokeo ya uhusiano huo katika nyanja za kijamii, kiuchumi na kisiasa.

6. Serikali ya Tanzania imegundua changamoto kubwa ya kuporomoka kwa maadili miongoni mwa vijana wa sasa, hivyo, imeamua kurejea katika mifumo ya jadi ya maadili. Kwa kuzingatia historia ya Tanzania na maadili, eleza chimbuko la maadili ya jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni na umuhimu wake katika kuongoza maisha ya jamii ambayo yanaweza kutumika hata sasa kwa kutumia hoja sita.

7. Katika mjadala wa kitaaluma kuhusu ukoloni, hoja imetolewa kuwa "elimu ilikuwa silaha kuu ya wakoloni kuliko bunduki." Kwa kutumia hoja sita, thibitisha kauli hii kwa kufafanua kwa kina jinsi elimu ilivyotumika kama nguvu laini wakati wa ukoloni nchini Tanzania kwa kutumia hoja sita.

shulelibrary.com

2

HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI

MTIHANI WA KIDATO CHA TANO

Muda: Saa 3

Maelekezo

1. Mtihani huu una maswali **saba (7)**.
2. Jibu maswali **matano (5)** tu. Swali la **kwanza (1)** ni la lazima.
3. Kila swali lina alama 20.
4. Maandishi yote yawe kwa wino **mweusi** au **bluu, isipokuwa** michoro, iwe kwa penseli.

Jibu Maswali **Matano (5)**. Swali la **kwanza (1)** ni la lazima.

1. Katika kijiji cha Chanzuru watu hawana uelewa kuhusu tunu za taifa la Tanzania. Wewe kama mwanafunzi wa somo la Historia ya Tanzania na Maadili mwenye maarifa ya tunu za taifa utawasilisha hoja zipi sita kwao?

2. Serikali imeamua kuendeleza eneo la Kilwa Kisiwani na Bagamoyo kwa kuweka miundombinu mizuri ya utalii na wananchi wameanza kunufaika. Kwa kutumia hoja sita, jadili namna wananchi watakavyonufaika na uendelezaji wa maeneo hayo.

3. Fafanua kwa hoja sita namna utalii wa urithi wa kihistoria unavyosaidia kuimarisha uhusiano wa kidiplomasia kati ya Tanzania na mataifa mengine.

4. Katika jamii moja nchini, wazazi wamegundua kuwa vijana wengi wamepoteza maadili kutokana na kuiga tamaduni za kigeni. Hivyo, wameamua kufufua elimu ya jadi kama jando na unyago. Jadili mambo sita yanayoweza kuigwa na kuendelezwa kutoka katika elimu ya jadi.

5. Kabla ya ukoloni, wafanyabiashara wa Kiarabu walifika pwani ya Tanzania na kufanya biashara na wenyeji. Hali hii ilisababisha mwingiliano mkubwa wa kijamii na kiuchumi. Unafikiri ni sababu gani sita zilichangia uhusiano kati ya jamii hizo?

6. Eleza mambo sita yaliyochangia mabadiliko ya maadili kutokana na uhusiano wa kihistoria.

7. Kabla ya ukoloni, jamii za Kitanzania zilikuwa na namna zao za kuhakikisha maadili yanafuatwa na kuheshimiwa na wanajamii wote. Kama mtaalamu wa historia ya Tanzania na maadili, chambua mifumo iliyotumika katika usimamizi wa maadili hayo kwa hoja sita.

Shulelibrary.com

3

HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI

MTIHANI WA KIDATO CHA TANO

Muda: Saa 3

Maelekezo

1. Mtihani huu una maswali **saba (7)**.
2. Jibu maswali **matano (5)** tu. Swali la **kwanza (1)** ni la lazima.
3. Kila swali lina alama 20.

4. Maandishi yote yawe kwa wino **mweusi** au **bluu, isipokuwa** michoro, iwe kwa penseli.

Jibu Maswali **Matano (5)**. Swali la **kwanza (1)** ni la lazima.

1. Katika semina ya kitaifa kuhusu uongozi bora, wataalamu wamejadili maadili ya viongozi wa chama na serikali yaliyoanishwa katika Azimio la Arusha. Baadhi ya vijana wanahoji kama maadili hayo bado yana umuhimu katika uongozi wa sasa. Onesha hoja sita ambazo wataalamu walizijadili.

2. Serikali imeanzisha kampeni ya kulinda urithi wa Taifa huku ikisisitiza umuhimu wa maadili katika matumizi ya rasilimali za kihistoria. Hata hivyo, baadhi ya maeneo ya urithi yanaharibiwa kutokana na kukosekana kwa maadili. Fafanua uhusiano kati ya maadili na urithi katika kuleta maendeleo ya taifa kwa kutumia hoja sita.

3. Katika juhudi za kukuza uchumi wa taifa, Tanzania imeendelea kuimarisha utalii wa kihistoria katika maeneo kama Kilwa, Bagamoyo na Zanzibar. Serikali imebaini kuwa utalii huu una mchango mkubwa katika biashara za kimataifa. Kwa utaalamu wako, tumia hoja sita kuelezea mchango wa urithi wa kihistoria katika sekta hiyo kimataifa.

4. Linganisha mifumo ya uongozi wa jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni na mifumo ya uongozi ya sasa nchini.

5. Katika dunia ya sasa, jamii za Tanzania zimeendelea kushirikiana na jamii nyingine kupitia biashara, elimu na teknolojia. Hata hivyo, hali hii ina mizizi yake katika historia ya mahusiano ya jamii. Eleza sababu sita za uhusiano kati ya jamii za sasa za Kitanzania na jamii nyingine.

6. Kama mtaalamu wa malezi na masuala ya vijana, umealikwa katika kongamano la wazazi kuelezea mada ya sababu za mabadiliko ya maadili kutoka kipindi kimoja hadi kingine. Onesha hoja sita ambazo utawasilisha mbele ya wazazi hao.

7. Katika historia ya Tanzania, viongozi mbalimbali walijitokeza kupambana dhidi ya vitendo vilivyohatarisha maadili ya jamii na taifa kwa ujumla. Fafanua kwa hoja sita namna viongozi wa jamii za Kitanzania walivyopambana ili kuyalinda maadili ya taifa.

4

HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI

MTIHANI WA KIDATO CHA TANO

Muda: Saa 3

Maelekezo

1. Mtihani huu una maswali **saba (7)**.
2. Jibu maswali **matano (5)** tu. Swali la **kwanza (1)** ni la lazima.
3. Kila swali lina alama 20.
4. Maandishi yote yawe kwa wino **mweusi** au **bluu, isipokuwa,** michoro iwe kwa penseli.

Jibu Maswali **Matano (5)**. Swali la **kwanza (1)** ni la lazima.

1. Katika maadhimisho ya Siku ya Uhuru wa Tanganyika, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alisisitiza mambo yanayowafanya Watanzania wajivunie taifa lao mbele ya mataifa mengine. Kwa kutumia maarifa uliyoyapata kwenye somo la Historia ya Tanzania na Maadili, unadhani ni mambo gani sita ambayo Mheshimiwa Rais aliyaeleza?

Shulelibrary.com

2. Katika kijiji fulani kilicho karibu na eneo la kihistoria, baadhi ya wananchi wamekuwa wakiharibu mazingira na miundombinu ya urithi kwa kukosa uelewa wa umuhimu wake. Kama mtaalamu wa historia na urithi, tumia hoja sita kueleza wajibu wa raia mmojammoja katika uhifadhi wa urithi.

3. Wizara ya Maliasili na Utalii imeandaa safari ya wanafunzi kutembelea makumbusho mbalimbali nchini ili kujifunza historia ya taifa. Kwa kutumia hoja sita, onesha makumbusho sita ambayo wanafunzi hao watayatembelea.

4. Kwa kutumia hoja sita, fafanua jinsi maadili yalivyochochea maendeleo katika jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni.

5. Pendekeza mikakati sita ya kuimarisha uhusiano kati ya jamii za Kitanzania na jamii nyingine za Afrika.

6. Katika mkutano wa viongozi wa dini na jamii, hoja iliibuliwa kuhusu mchango wa dini katika kukuza maadili ya Kitanzania. Kwa kutumia hoja sita, eleza michango hiyo.

7. Fafanua maadili sita yaliyojengwa wakati wa ukoloni nchini Tanzania.

5

HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI

MTIHANI WA KIDATO CHA TANO

Muda: Saa 3

Maelekezo

1. Mtihani huu una maswali **saba (7).**
2. Jibu maswali **matano (5)** tu. Swali la **kwanza (1)** ni la lazima.
3. Kila swali lina alama 20.
4. Maandishi yote yawe kwa wino **mweusi** au **bluu, isipokuwa,** michoro iwe kwa penseli.

Jibu Maswali **Matano (5)**. Swali la **kwanza (1)** ni la lazima.

1. Eleza kwa kutumia hoja sita namna Muungano wa Tanganyika na Zanzibar unavyoakisi maadili ya taifa la Tanzania.

2. Chambua kwa kutumia hoja sita wajibu wa serikali ya Tanzania katika uhifadhi wa urithi wa taifa.

3. Eleza changamoto sita za kimaadili zinazoweza kuathiri maendeleo ya jamii na taifa kwa ujumla.

4. Serikali ya Tanzania ina vyombo na taasisi mbalimbali za kuhifadhi na kuendeleza urithi wa taifa, mojawapo ni Idara ya Makumbusho ya Taifa na Mambo ya Kale. Ukiwa kama afisa wa wizara ya utalii, eleza majukumu sita ya Idara hiyo.

5. Katika mjadala wa kitaifa kuhusu lugha, imeelezwa kuwa Kiswahili si tu lugha ya mawasiliano, bali ni chombo muhimu cha kujenga maadili ya jamii za Kitanzania. Thibitisha hili kwa hoja sita.

6. Fafanua kwa kutumia hoja sita namna elimu ilivyotumika kueneza utamaduni wa kikoloni nchini Tanzania.

7. Eleza kwa kutumia hoja sita maadili yaliyojengwa katika jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni.

shulelibrary.com

6

HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI

MTIHANI WA KIDATO CHA TANO

Muda: Saa 3

Maelekezo

1. Mtihani huu una maswali **saba (7)**.
2. Jibu maswali **matano (5)** tu. Swali la **kwanza (1)** ni la lazima.
3. Kila swali lina alama 20.
4. Maandishi yote yawe kwa wino **mweusi** au **bluu, isipokuwa,** michoro iwe kwa penseli.

Jibu Maswali **Matano (5)**. Swali la **kwanza (1)** ni la lazima.

1. Wizara ya Utamaduni imeanzisha kampeni ya kitaifa ya kuimarisha matumizi ya lugha ya Kiswahili ili kulinda utambulisho wa taifa. Kama mtaalamu wa historia ya Tanzania na maadili, tumia hoja sita kueleza namna lugha ya Kiswahili ilivyochangia katika kuimarisha utambulisho na maadili ya taifa la Tanzania.

2. Pendekeza njia bora sita za uhifadhi wa urithi wa taifa kwa maendeleo endelevu.

3. Serikali imepokea taarifa kuwa baadhi ya vivutio vya kihistoria vinaharibiwa na kupoteza thamani yake kutokana na usimamizi mbovu. Tathmini athari sita zinazoweza kutokea iwapo Tanzania itashindwa kusimamia vema vivutio vya kihistoria na urithi wake.

4. Taifa letu linakumbwa na changamoto kubwa za kimaadili ambazo zinakuwa kikwazo katika kuleta maendeleo. Kama mwanafunzi mwenye maarifa kwenye masuala ya maadili, fafanua changamoto hizo kwa kutumia hoja sita.

5. Wangoni ni moja ya makabila ya Tanzania ambayo yalileta athari nyingi sana pindi walipoingia kutokea Afrika Kusini. Ukiwa umepewa jukumu la kuwasilisha mada hii mbele ya wanafunzi wenzako darasani, zipi zitakuwa hoja zako sita?

6. Jadili matokeo sita hasi ya mapokeo kati ya jamii za Kitanzania na zile za kigeni.

7. Kutawaliwa kwa jamii za Kitanzania na wakoloni ni matokeo ya msukumo wa mambo mbalimbali. Elezea msukumo huo kwa kutumia hoja sita.

Shulelibrary.com

7

HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI

MTIHANI WA KIDATO CHA TANO

Muda: Saa 3

Maelekezo

1. Mtihani huu una maswali **saba (7)**.

2. Jibu maswali **matano (5)** tu. Swali la **kwanza (1)** ni la lazima.
3. Kila swali lina alama 20.
4. Maandishi yote yawe kwa wino **mweusi** au **bluu, isipokuwa,** michoro iwe kwa penseli.

Jibu Maswali **Matano (5)**. Swali la **kwanza (1)** ni la lazima.

1. Katika warsha ya viongozi vijana, umealikwa kama mtaalamu wa masuala ya uongozi kutoa mada kuhusu namna tunu za taifa zinavyojenga misingi ya uongozi bora. Onesha hoja zako sita utakazozizungumza mbele ya vijana hao.

2. Kwa kutumia hoja sita na mifano, fafanua changamoto zinazokabili uhifadhi wa urithi wa taifa.

3. Serikali ya Tanzania imekuwa ikichukua hatua mbalimbali kuboresha vivutio vya kihistoria ili kuongeza utalii na maendeleo ya taifa. Kama mshauri wa wizara ya maliasili na utalii, eleza hatua sita zilizochukuliwa na serikali kufanikisha hilo.

4. Katika utafiti wake wa historia ya jamii za Kitanzania, Makanja amebaini kuwa kabla ya ukoloni kulikuwa na mifumo madhubuti ya kusimamia maadili. Chambua mifumo hiyo na namna ilivyosaidia kudumisha maadili katika jamii.

5. Eleza athari sita za ujio wa Wangoni katika jamii za Kitanzania.

6. Kabla ya ukoloni, jamii za Kitanzania zilipitia mabadiliko ya maadili kutokana na mwingiliano wa kihistoria. Fafanua mabadiliko sita yaliyopitiwa.

7. Wataalamu wengi wa historia ya Tanzania wanadai kuwa wakoloni walichangia kwa kiasi kikubwa kumomonyoka kwa maadili ya jamii za Kitanzania. Jadili sentensi hii kwa hoja sita.

Shulelibrary.com

8

HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI

MTIHANI WA KIDATO CHA TANO

Muda: Saa 3

Maelekezo

1. Mtihani huu una maswali **saba (7)**.
2. Jibu maswali **matano (5)** tu. Swali la **kwanza (1)** ni la lazima.
3. Kila swali lina alama 20.
4. Maandishi yote yawe kwa wino **mweusi** au **bluu, isipokuwa,** michoro iwe kwa penseli.

Jibu Maswali **Matano (5)**. Swali la **kwanza (1)** ni la lazima.

1. Fafanua kwa hoja sita namna alama za taifa zinavyotumika kudumisha maadili ya taifa la Tanzania.

2. Katika tamasha la urithi lililofanyika katika mji wa Bagamoyo, wananchi walifundishwa njia bora zinazoweza kutatua changamoto za uhifadhi wa urithi wa taifa kwa maendeleo endelevu. Unafikiri wananchi walifundishwa njia gani? Tumia hoja sita kufafanua.

3. Watanzania wengi hawazijui fursa za kiuchumi zinazotokana na kuhifadhi urithi wa kiutamaduni katika maeneo yao. Waelimishe fursa hizo kwa kutumia hoja sita.

4. Tangu enzi na enzi, elimu imekuwa msingi muhimu wa maendeleo ya nchi yoyote. Hata hivyo, baadhi ya wananchi bado hawajaelewa mchango wake kikamilifu. Fafanua kwa kwa kutumia hoja sita mchango wa elimu katika kuleta maendeleo nchini Tanzania.

5. Historia ya Wangoni imekuwa ya kuvutia na kushangaza sana kutokana na uimara wao na kuzishinda jamii nyingi kwa kupigana na hatimaye kuanzisha makazi yao. Eleza sababu sita za Wangoni kupata ushindi huo.

6. Katika utafiti wa kijamii, imebainika kuwa mwingiliano wa jamii za Kitanzania na wageni umechangia kwa kiasi kikubwa mabadiliko ya maadili katika jamii. Jadili kwa hoja sita uhusiano uliopo kati ya mmomonyoko wa maadili na ujio wa wageni katika jamii za kitanzania.

7. Ni ukweli usiopingika kwamba ukoloni uliathiri sana mfumo wa maadili wa jamii za kitanzania. Fafanua Athari hizo kwa kutumia hoja sita.

9

HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI

MTIHANI WA KIDATO CHA TANO

Muda: Saa 3

Maelekezo

1. Mtihani huu una maswali **saba (7)**.
2. Jibu maswali **matano (5)** tu. Swali la **kwanza (1)** ni la lazima.
3. Kila swali lina alama 20.
4. Maandishi yote yawe kwa wino **mweusi** au **bluu, isipokuwa,** michoro iwe kwa penseli.

Jibu Maswali **Matano (5)**. Swali la **kwanza (1)** ni la lazima.

1. Katika kongamano la kitaifa kuhusu utambulisho wa Tanzania, wanafunzi walipewa jukumu la kuchambua vyombo na taasisi zinazolinda historia, utambulisho na maadili ya taifa. Eleza vyombo na taasisi hizo kwa hoja sita.

2. Wewe ni mtumishi katika Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, umepewa jukumu la kuandaa ripoti kuhusu mchango wa teknolojia katika uhifadhi wa urithi wa taifa. Onesha hoja zako sita utakazoziandika katika ripoti yako.

3. Katika eneo la kihistoria la Kilwa Kisiwani, imeonekana baadhi ya watu wanajihusisha na vitendo vinavyoharibu urithi. Kama mkereketwa wa utamaduni, eleza vitendo sita visivyo vya kimaadili vinavyodumaza fursa zitokanazo na urithi.

4. Kwa kutumia hoja sita, eleza nafasi ya maadili katika kuchochea maendeleo.

5. Kama mwanafunzi wa Historia ya Tanzania na Maadili, umepewa kazi ya kueleza chimbuko la biashara kati ya jamii za Mashariki ya Kati na Mbali na jamii za Kitanzania. Eleza kwa kwa hoja sita chimbuko hilo.

6. Wewe ni kiongozi wa dini katika jamii yako, umeombwa kueleza mchango wa dini katika kujenga maadili ya jamii za Kitanzania. Toa hoja sita zenye maelezo ya kina kuhusu jambo hilo.

shulelibrary.com

7. Bw. Mpwimbwe ni mwalimu mzoefu wa somo la Historia ya Tanzania na Maadili, ameombwa kueleza umuhimu wa vita vya Majimaji katika historia ya Tanzania mbele ya wananchi katika maadhimisho ya siku ya mashujaa wa Tanzania. Jadili kwa kina hoja zake sita atakazoziwasilisha.

10

HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI

MTIHANI WA KIDATO CHA TANO

Muda: Saa 3

Maelekezo

1. Mtihani huu una maswali **saba (7)**.
2. Jibu maswali **matano (5)** tu. Swali la **kwanza (1)** ni la lazima.
3. Kila swali lina alama 20.
4. Maandishi yote yawe kwa wino **mweusi** au **bluu, isipokuwa,** michoro iwe kwa penseli.

Jibu Maswali **Matano (5)**. Swali la **kwanza (1)** ni la lazima.

1. Pendekeza mikakati sita ya kuhifadhi historia ya taifa la Tanzania kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

2. Serikali imeanza kampeni ya kukuza uchumi kupitia sekta ya utalii wa kihistoria. Imesisitiza kuwa historia na urithi wa taifa vina mchango mkubwa katika uchumi imara na endelevu nchini Tanzania. Eleza mchango huo kwa hoja sita.

3. Ripoti ya mdhibiti na mkaguzi wa hesabu za serikali imeonesha uwepo wa matumizi mabaya ya rasilimali za urithi wa kiutamaduni katika baadhi ya maeneo ya kihistoria. Eleza hatua ambazo serikali inaweza kuchukua ili kuhakikisha kunakua na uwajibikaji katika matumizi ya rasilimali hizo.

4. Katika mjadala wa kitaaluma, wanafunzi wamebaini kuwa maadili ya jamii za Kitanzania yamebadilika sana kutoka kipindi cha kabla ya ukoloni hadi sasa. Chambua kwa hoja sita tofauti za kimaadili zilizopo katika jamii za Kitanzania katika vipindi hivyo viwili.

5. Fafanua kwa kutumia hoja sita changamoto zilizokuwepo katika biashara kati ya jamii za kitanzania na zile za mashariki ya Kati na Mbali.

6. Chukulia wewe ni kiongozi wa kanisa na umealikwa na umoja wa wazazi Tanzania kuelezea mada ya mchango wa dini ya kikristo katika kujenga maadili ya sasa. Unafikiri utaeleza hoja gani sita mbele ya wazazi hao?

7. Watangulizi wa ukoloni walisaidia sana kuanzishwa na kuimarika kwa ukoloni nchini Tanzania. Kwa kutumia hoja sita, fafanua msaada wao katika kuanzisha na kuimarisha ukoloni.

shulelibrary.com